TANGAZO LA SERIKALI Na. 44 la tarehe. 24/1/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAEGESHO YA HALMASHAURI YA MJI WA HANDENI YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Maegesho ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2025.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmshauri ya Mji wa Handeni.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilkanuni ya Handeni;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilkanuni ya Mji wa Handeni au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru wa maegesho" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa kuegesha chombo cha usafiri katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa maegesho

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya vyombo vya usafiri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadiri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, Halmashauri itatenga na kuainisha maeneo ya maegesho kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri.

(5) Mtu yeyote anayetumia chombo cha usafiri atakuwa na wajibu wa kuegesha chombo hicho katika maegesho yaliyoainishwa na kulipa ushuru wa maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Namna ya kutoza ushuru wa maegesho

**5**.-(1) Ushuru wa maegesho utatozwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kila siku.

(2) Ushuru wa maegesho utatozwa kwa kila chombo cha usafiri ndani ya saa ishirini na nne au kwa mwezi kadri Halmashauri au mlipa ushuru atakavyoona inafaa.

(3) Mtu yeyote atakayetozwa na kulipa ushuru wa maegesho atapewa stakabadhi ya kielektroniki.

(4) Mtu yeyote atakayelipa ushuru wa maegesho kwa siku au mwezi ataruhusiwa kuegesha chombo cha usafiri alicholipia katika eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya maegesho kwa muda aliolipia bila kutozwa tena.

(5) Chombo cha usafiri kinachomilikiwa na Serikali, Jeshi au Ubalozi hakitatozwa ushuru wa maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu na uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

**6**.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata, kukifunga kwa kifaa maalum na kuondoa chombo cha usafiri kilichoegeshwa katika eneo ambalo halijaainishwa au kutengwa kwa ajili ya maegesho.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) kitaondolewa na kuhifadhiwa katika yadi ya Halmashauri au eneo lolote lililoainishwa na Halmsahuri.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo cha usafiri baada ya kupata amri ya mahakama endapo mmiliki hatajitokeza au atashindwa kulipa gharama anazodaiwa ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kukamatwa.

Maegesho maalumu

**7**.-(1) Halmashauri inaweza kutenga eneo maalumu la barabara ya Halmashauri kwa ajili ya maegesho ya malori na vyombo vingine vya usafiri na kutoza ushuru wa maegesho kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 6(1) ya Sheria Ndogo hii, muda wa kuegesha chombo cha usafiri katika maegesho maalumu utapangwa kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa wakala

**8**.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa madhumuni ya kukusanya ushuru wa maegesho kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru wa maegesho kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru wa maegesho kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa

**9**. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote-

(a) atakayeshindwa kulipa ushuru wa maegesho;

(b) atakayeegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaainishwa au kutengwa kwa ajili ya maegesho;

(c) atakayegesha chombo cha usafiri bila kuzingatia alama zilizoainishwa kwenye maegesho;

(d) atakayeosha au kutengeneza chombo cha usafiri bila dharura katika eneo la maegesho au kufanya shughuli isiyo ya maegesho katika eneo la maegesho bila kibali;

(e) atakayeshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru wa maegesho;

(f) atakayefanya udanganyifu kwa madhumuni ya kukwepa ushuru; au

(g) atakayemzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii.

Adhabu

**10**. Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii na kutiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidishilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufililisha kosa

**11**. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kulipa ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

USHURU WA MAEGESHO

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru Kwa Siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Basi | 2,000/= |
| 2 | Gari la Kawaida | 500/= |
| 3 | Lori | 1,500/= |
| 4 | Noah | 500/= |
| 5 | Pick up | 500/= |
| 6 | Pikipiki yenye Magurudumu matatu au Bajaji | 300 /= |
| 7 | Pikipiki yenye Magurudumu mawili | 200/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

USHURU WA MAEGESHO MAALUMU

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru kwa Shilingi | |
|---|---|---|---|
| | | KWA SIKU | KULAZA |
| 1 | Bajaji | 3,000/= | 6,000/= |
| 2 | Basi | 5,000/= | 10,000/= |
| 3 | Fuso | 5,000/= | 10,000/= |
| 4 | Gari la kawaida | 3,000/= | 6,000/= |
| 5 | Lori bila tela | 5,000/= | 10,000/= |
| 6 | Lori lenye tela | 10,000/= | 20,000/= |
| 7 | Pikipiki | 2000/= | 4,000/= |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengezwa chini ya kanuni ya 11)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFLILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Maegesho ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Handeni, niko tayari kulipa faini ya ufifilishaji wa kosa ya kiasi cha shilingi ......................... na ushuru ninaodaiwa wa kiasi cha shilingi ........................

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:

Jina: …………………………………..……………………

Saini……………………….……………………………..………

Wadhifa: …………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………….

Nembo ya Halmashauri ya Mji Handeni imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji uliofanyika tarehe 7/2/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

MARYAM A. UKWAJU,
*Mkurugenzi wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji*
*Handeni*

MUSSA A. MKOMBATI,
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji,*
*Handeni*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
9 Disemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*